# LBE KOMPUTA NA INTANETI - Programme 4

Mwandishi: Richard Lough

Muhariri: Maja Dreyer

Tafsiri:Eric Ponda

**Wahusika:** Beatrice (Msichana wa makamu ), John (Mvulana wa makamu), Komputa (Sauti), Mtaalam (Sauti ya Mwanamume kutoka Studio)

Mark Sewe (Mvulana miaka 19 katika mkahawa wa Intaneti)

Msimulizi: Mmmoja kutoka Studio

**Muziki – [Full up for 0:10 then fade under Intro]**

## Intro:

Hujambo na karibu tena kwa makala ya Noa Bongo Jeng Maisha yako kuhusu masuala ya Komputa na Intaneti.. Katika kipindi hiki cha nne, Beatrice na John wamegundua ulimwengu wa barua-pepe kupitia mtandao wa Intaneti yaani ***Emails.*** Kila siku mamilioni ya barua pepe hutumwa kupitia mtandao wa Intaneti kote Ulimwenguni.
Siku hizi huduma za kutuma barua na faksi zimeanza kupitwa na wakati. Lakini barua-pepe ni nini, na ni vipi inavyofanya kazi?. Ungana nasi hadi mwisho wa kipindi ujifunze mengi kuhusu huduma hizi …

## Package 4.1

**SFX_mtandao wa Intaneti ukifunguliwa [Sauti ikitioweka chini kwa chini…]**

**1. Sauti ya Komputa:** Habari John na Beatrice…

**2. John/Beatrice:** Habari Komputa…

**Full Up SFX_ Mtandao ukifunguliwa**

**3. Komputa:** Subirini kidogo nikijiunganisha na mtandao wa Intaneti…. Sawa ..

**SFX_Mtandao waunganishwa**

**4. Komputa:** Sawa…sasa tumeunganishwa. Nimfanyie nini leo ?

**5. John:** Leo nilikuwa darasani na mwalimu wangu alishangaa sana kusikia kwamba sielewi maana ya baraua pepe au ***Email…..*** ni nini?.

**8. Komputa:** Sawa , nitakusaidia. Kwanza kabisa barua Pepe au ***Emails*** ni barua zinazotumwa kwa njia ya eletroniki..

**9. Beatrice:** Kwa hivyo bado tu ni Barua?

**10. Komputa:** Tunaweza kusema hivyo…Ila tu unatumia Komputa kuandika na kutuma barua hii.

**11. John:** Kisha unaituma na posta?

**12. Komputa:** *(kicheko)* Hapana, hapana! Kwanza unahitaji moja wapo ya hizi…

**SFX_Akipiga chama kwenye komputa.**

**13.Beatrice:** *[**akisoma pole pole**]* www.yahoo.com

**14.Komputa:** Kwanza unahitaji kuwa na akaunti yako ya barua pepe yaani ***Email*** …

**15. John:** Ni ghali ?

**16. Komputa:** Hapana, kuna kampuni nyingi tu zinazotoa huduma hizi bila malipo. Kama hii sasa ya ***Yahoo***. Pia kuna ile ya ***Hotmail*** na ***Gmail.***

**SFX_Akibonyeza Mouse mara moja**

**17. Komouta:** Sasa unabonyeza hapa mara moja ili kufungua akaunti yako . Kisha andika maelezo yako kamili, jina na kadhalika..

**SFX_Akiandika kwa Komputa**

**18. Komputa:** Sawa… Ni rahisi sana . Sasa mumefungua akaunti yanu: ***John na Beatrice at yahoo dot com…***

**19.Beatrice:** Sasa tuko tayari kutuma na kupokea barua pepe?

**20 Komputa:** Ndio….! Lakini kwanza bonyeza hapa kunasema ***'compose message'*** yaani andika barua.

**SFX_Akibonyeza Mouse_**

**21. John:** Sawa katika kijisanduki kuna maandishi ***`to´*** yaani kwa yule mtu unayemtumia. Kwa hivyo naweza kuandika jina la Mtu ninayetaka kumtumia barua hii?

**22. Komputa:** Hapana, kwanza ni lazima uandike anuani yake ya barua Pepe ***`Email`´*** . Unaweza tu kutuma barua hii kwa Mtu ambaye pia ana anuani au akaunti ya barua pepe.

**23. Beatrice:** Kwa mfano kakangu. anaitwa Nelson. ' yuko nchini Marekani na anuani yake ni ***hotmail dot com'.***

**SFXAkiandika kwa Komputa**

**25. Komputa:** Sawa . Na pia ukitaka, kwenye kijisanduki kidogo chini yake kuna maandishi yanayosema ***‘Subject’*** katika kijisanduki hicho unaweza kuandika tu kwa ufupi mada ya Barua hiyo.

**26. John:** Itakuwaje endapo utakosea anuani ya barua pepe ya yule unayemtumia.?

**SFX Sauti ya kuashiria makosa**

**27. Komputa:** Swali zuri sana. Ukikosea anuani , basi barua hiyo haitamfikia unayemkusudia. Ukituma barua hiyo kwa anuani isiyokuwepo barua hiyo itarudi tu na kukufahamisha kulitokea makosa, au anuani uliyotumia haimo au haijulikani..

**28. John:** So, Sasa huchukua muda gani barua kumfikia unayemkusudia?

**29. Komputa:** Ni papo hapo… Huu ndio uzuri wa kutumia barua pepe kuliko zile za kawaida. Hakuna malipo kutuma barua pepe , hakuna! Kwa hiyo ni rahisi kuliko hata kutumia Faski.

**30. Beatrice:** Kwa hivyo unaweze tu kupokea barua kutoka kwa Mtu anayekufahamu au kujua anuani yako?

**31. Komputa:** Ndio . Lakini kwa mtandao wa Intaneti hakuna hakikisho thabiti kwamba anuani yako ni salama …

**32. John:** Hakuna usalama?

**33. Komputa:** Hakuna, lakini suala hili tutalizungumzia kwa kina baadaye.

**34. Beatrice:** Kwa hivyo watu wengine wanaweza kutumia anuani yako?

**35. Komputa:** Ndio wanaweza. Hao ni watu ambao utakuta wanatuma barua taka kwa anuani yako kila mara.

**36. Beatrice:** Barua taka?!

**37. Komputa:** Barua nyingi tu zisizo na maana …. Mara nyingi barua hizi hutumwa kwa watu wengi tu, na mwenye kutuma barua hizi mara nyingi hutumia anuani ya wizi ambayo si yake.

**SFX_Beep [kuashiria Barua imepokewa ]**

**38. Komputa:** Unaona sasa… Hii inaonekana kama moja wapo ya barua tunazozungumzia.

**39. John:** Verlinda Kwani… Hatumjui Verlinda!.

**40. Komputa:** Hasa...! Labda pengina hakuna Mtu anayeitwa kwa jina hili… hebu twende chini tusome zaidi barua hii…

**SFX_ Bonyeza Mouse**

**41. Beatrice:** Wanauza madawa. Si inaudhi sana kupokea barua kama hizi zinazojaza akaunti yako tu!!

**42. John:** Kwani hakuna njia unavyoweza kuzuia barua hizi?

**43. Komputa:** Unaweza. Lakini si rahisi kuzuia takataka zote zinazotumwa kwa anuani yako. Unaweza kununua aina ya programu au data inayoweza kuzuia na takataka hizi . Lakini data hii huwa na mambo mengi kuliko ile inayopatikana kwa mtandao wa Intaneti

**Music – Full up for 0:10 then fade under**

**SFX_Katika mkahawa wa EasySurf**

**1. John:** Habari Mark, … unatafuta nini?

**Clip: 4.2_Mark_1**

Ninawasiliana moja kwa moja na Marafiki zangu kwa kutumia mtandao wa ***Skype***

**2. John:** Sawa ***(hana hakika***)

**SFX_Mark_Skyping [Full up to 0:08 for dialling tone then fade under]**

**3. John:** Ni kama ile sauti ya simu tu….! Sikudhania ni kama simu ya kawaida

**Keep SFX_Ambie_EasySurf and SFX_Mark_Skyping as sound bed throughout.**

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**4. Mtaalam :** John, huyu ni mtaalam wako , hebu nikusaidie. Programu anayotumia Mark inaitwa ***Skype***. Huduma hizi zinakuwezesha kuzungumza moja kwa moja kupitia mtandao wa Intaneti. Unaweza kuwapigia marafiki zako, na kama wana akaunti na mtandao huu wa ***skype***, ambao ni sawa na akaunti ya ***Email*** unaweza kuwapigia simu moja kwa moja kutoka kwa komputa yako.

**5. John:** Mark, umekuwa ukizungumza na Dadako Easther. Nani mwengine unataka kuzungumza naye kupitia ***Skype***?

**Clip: 4.2_Mark_2**

Wakati mwingi hutumia ***skype*** kuzungumza na Kakangu ambayo yuko nchini Ukraine, alienda huko miaka mitatu iliyopita..

**6. John:** Je unahitaji vifaa maalum kutumia mtandao huu wa ***Skyper ?***

**Clip: 4.2_Mark_3**

Ili kutumia mtandao huu wa skype, unahitaji spika ndogo za kuweka kwenye masikio na pia Mikrofoni ndogo … Siku hizi nyingi ya mikahawa inavifaa hivi, na huu ndio uzuri wake.

**7. John:** Lakini kwanini utumie ***Skype*** kuzungumza na Kaka yako na wala sio siimu ya kawaida au ile ya mkononi?

**Clip: 4.2_Mark_4**

Nilijaribu kutumia simu yangu ya mkononi na hata ile la kawaida lakini ni ghali mno ikilinganisha na huduma hizi za.

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**8. Mtaalam :** Hebu nikukatize tena kidogo, nikifahamishe gharama za huduma hizi za…

**9. John** Endelea Mtaalam.

**10.Mtaalam** Kwanza kuna Data –na programu nyingine kama hizi zinazopatikana bila malipo. Wakati unapotumia huduma hizi kumpigia simu Mtu mwengine aliye na akaunti na mtando huu, basi unaweza kufanya hivyo bila malipo. Unagharamia tu huduma za kuunganishwa . Na iwapo utapiga simu, gharama hutegemea na nchi unakopiga simu hiyo. Kwa mfano ukipiga simu nchini Uingereza au Marekani gharama yake ni nafuu zaidi kuliko kupiga nchini Somalia.Kugharamia malipo ni lazime uweke pesa kwenye akaunti yako. Unaweza kufanya hivyo kwa kununua kadi ya pesa.

**9. John:** Ni jambo la kustaajabisha. Nimejifunza kuhusu barua pepe yaani ***Emails*** na jinsi unavyoweza kuwatumia watu barua kwa upesi , Na sasa nimejifunza jinsi ninavyoweza kuongea na watu kupitia mtandao .

**10.** Mtalaam**:** Hasa si lazime utumie sauti yako kuwasiliana na Mtu. Unaweza kuingia sehemu inayojulikana kama chumba cha mawasiliano yaani ***Chat room***.

**11.John** Chumba au Chat room ni nini ?

**12. Mtaalam** Ni sehemu unapoweza kutumia mtandao kuwasiliana na watu kwa kuwandika ujumbe kwenye komputa yako. Hapo munawasiliana moja kwa moja na mwenzako kama vile Mark Sewe alivyokuwa akitueleza hapo awali .

**13. John:** Kwa hivyo unaonaje huduma hii ya kuzungumza moja kwa moja na Kakako ?

**Clip: 4.2_Mark_6**

Nimeifurahuia sana, inaonekana ni kana kwamba ulimwengu umekuwa kijiji, hata kama mwenzako yuko pembe nyingine ya ulimwengu unaona kama yuko tu karibu.

**Outro**

Na ni hayo tu tuliyoweza kumuandalia kwa kipindi cha leo, ambapo tumejifunza mengi kuhusu mawasiliano ya moja kwa moja kupitia mtandao wa Intaneti. Lakini kumbuka unahitaji huduma nzuri za kukuunganisha kwenye Intaneti, spika na Mikrofoni ndogo ili uweze kutumia vyema huduma hizi za ***Skyper*** au nyinginezo za mawasiliano ya papo kwa papo. Iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki pamoja na rafiki zako, unaweza kutembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa.

**Mwisho**